EQUALISM

Usawa ni mfumo wa uchumi ambao huhakikisha kwamba rasilimali za jamii husika huinafaisha jamii katika ujumla wake na sio mtu mmoja mmoja
mfumo wa usawa husimamia ugawanaji wa rasilimali zinazopatikana katika jamii husika kwa namna iliyo bora kabisa. Mfumo huu huhakikisha kwamba kila mwanajamii aliezaliwa katika jamii husika anayo haki ya kupata mahitaji yake ya msingi maadamu anatimiza wajibu wake katika jamii.
Katika mfumo wa usawa kufanikiwa sio haki ya wachache bali moja kwa moja kila anayefanya kazi na kutimiza wajibu atakuwa amesha fanikiwa. Hii ni kwasababu watu wote waliochini ya mfumo wa usawa hupata kipaumbele sawa bila kuweka matabaka ya aina yoyote ile. Mfumo wa usawa kama jina lake lilivyo ni dawa ya matabaka katika jamii. Mfumo huu huwezekana endapo nchi au dunia kwa ujumla wake watatambua kuwa kila mtu aliyezaliwa anayohaki ya kuishi maisha mazuri yasiyo na hali ya aina yoyote ile ya kinyonyaji.
Katika mfumo wausawa kila mtu ni tajiri hakuna maskini hata mmoja.

MGAWANYO WA RASILIMALI

Duniani zipo rasilimali nyingi sana. Huwezi kusema kwamba baadhi ya watu ni maskini kwasababu rasilimali hazitoshi. Rasilimali za duniani zinatutosha na ndio maana wote tunaishi. Hii ni kkwa sababu uhaba wa rasilimali muhimu ungepelekea kufariki kwa baadhi ya watu wa kipato cha chini. Tatizo liko katika ugawanyaji wa rasilimali hizo. Baadhi ya watu wanajilimbikizia rasilimali muhimu na kuwaacha wengine wakiishi maisha ya kuunga unga. Utakuta mtu mmoja anautajiri unaotosha kuwalisha watu elfu kumi kwa muda wa mwaka mmoja bila wao kufany chochote wakati wapo watu ambao chakula chao ni cha kubahatisha. Watu hupenda kukusanya malikwa wingi ili kujitenga na wasiwasi wakukosa katika siku za mbeleni. Katika mfumo wa usawa raia hawatakuwa na hofu ya maisha yao ya kesho kwa hiyo hakuna haja ya kulimbikiza mali. Mfumo wa usawa umekuja na njia bora kabisa ya kugawana rasilimali katika hali ya usawa kwa jamii nzima na kuufanya umaskini kuwa ni historia katika uso wa dunia. mfumo wa usawa . Mfano chakula kinacholimwa dunia kinatutosha wote, endapo utatokea ukama sehemu moja basi sehemu nyingine ya dunia wanavuna vizuri. Mfumo wa usawa husimamia pia ueneaji wa rasilimali kutoka sehemu ambayo zimezalishwa kufika sehemu nyingine bila gharama yoyote zaidi ya nguvu za wanadamu

JINSI NILIVYO UGUNDUA

Nimegundua mfumo huu baada ya kusoma maandiko matakatifu ya quran yanayozungumzia habari za peponi. Nikavuta picha ya sehemu yenye kila kitu kinachohitajika. Sehemu ambayo rasilimali ziko kwa wingi kushinda watumiaji. Kwa mujibu wa quran pepo ni bustani yenye mito, maziwa, asali, matunda na nyama za ndege. Mbali na hayo kuna wanawake waliotakaswa na watumishi ambao ni vijana wadogo wasiozeeka. Baada ya kusoma habari hii nikavuta picha ya bustani hii nikitumia upeo wangu wa kufahamu mazingira ya dunia ndipo nikagundua kuwa hata dunia ni bustani yenye mito, maziwa, asali na wanyama wengi ambao ni kitoweo na wengine huvutia kutizama. Basi nafsi yangu ikatamani kupata maisha kama yale hapa duniani wakati najiandaa kwa ajili ya maisha ya huko peponi. Ndipo nilipogundua mfumo wa usawa ambao tunaweza tukaisha maisha ambayo ni taswira ya maisha ya huko peponi. Peponi hakuna biashara wala matumizi ya fedha. Na ilikuwa hivyo hata mwanzo wa ulimwengu wakati wanadamu ni wachache. Katika mfumo wa usawa wanadamu huishi maisha kama wako katika bustani ya edeni (firdaus), tofauti ni kwamba itawabidi wafanye kazi ili maisha hayo yawe ya kudumu na sio ya muda mfupi.

UZALISHAJI

Katika mfumo wausawa hakuna biashara wala matumizi ya fedha, hii itapelekea kupungua kwa nafasi za kazi kwa zaidi ya asilimia 60. hii ni kwasababu mambo mengi ambayo mwanadamu wa leo

anayaendesha hutegemea biashara. Kila mtu hujitahidi awe na bidhaa ya kuuza au ujuzi ili aweze kubadilisha kwa fedha. Mfumo wa usawa utakapo anza kutumika utafuta mambo ya biashara na matumizi ya fedha mara moja. Kazi zitakazo bakia ni zile za kushughulika na rasilimali za asili au kuhudumia watu. Lengo kubwa la mfumo wa usawa ni kupunguza nafasi za kazi ambazo sio za muhimu ili mwanadamu apate kupunzika na mbio za usakaji maisha. Kazi zikiwa chache watu watazifanya kwa zamu hivyo watapata muda mwingi wa kumtukuza mungu na kustarehe. Hii ndio taswira ya edeni. Uzalishaji utaongezaka kwa sababu nguvu kazi itakuwa imeelekezwa moja kwa moja katika rasilimali asili na sio katika kusaka pesa.

KAZI YA PESA

Kwa mujibu wa mfumo wa usawa fedha ni kama nguvu kuu (force) inayo walazimisha watu wafanye kazi kwa bidii ili wapate bidhaa au ujuzi wa kubadilishana moja kwa moja wapate pesa. Mtu mwenye maisha mazuri ni yule mwenye uwezo mkubwa wa kufanya manunuzi. Hakuna watu ambao huzalisha bidhaa zote muhimu wanazohitaji kwa hiyo fedha imesaidia katika kubadilishana bidhaa. Japo fedha ni muhimu katika maisha ya mwanadamu lakini fedha imekuwa chombo muhimu sana katika unyonyaji. Kwa kutumia fedha katika kuuza na kununua bidhaa hufanyika ulanguzi wa hali ya juu sana na muadhirika mkuu ni mlaji wa mwisho katika kununua bidhaa hiyo. Kwa kutumia fedha mtu anaweza akafanya kazi kwa bidii lakini asipate faida na mjanja fulani akapata faida kubwa kwa sababu tu anajishughulisha na kazi za uuzaji au udalali. Mfano mkulima amelima kwa bidii sana na kutoa mazao bora lakini soko likiyumba basi atapata hasara kubwa ili mfanyabishara apate faida.

JINSI UNAVYOFANYA KAZI

Mfumo wa usawa huwataka watu wafanye kazi kwa bidii. Hii ni kwa sababu endapo watu wataacha kufanya kazi maisha ya wanadamu yatakuwa yamefikia ukingoni. Kila mtu mwenye afya ambaye sio mwanafunzi atalazimika kufanya kazi. Baada ya kazi hakuna mshahara kwa sababu katika mfumo wa usawa kufanya kazi ni kutimiza wajibu. Baada ya kazi atapatiwa utambulisho utakao muwezesha yeye kwenda dukani kuchukua mahitaji yake ya muhimu. Mfumo huu huhitaji kuwepo kwa duka moja kubwa (super market) katika kila mtaa. Duka ambalo litakuwa limesheni bidhaa zote za muhimu zinazohitajika kwa maisha ya kila siku. Watu wa mtaa huo watakuwa wanakwenda dukani kuchukua bidhaa zao bure bila malipo ya aina yoyote. Ambaye hakutimiza wajibu hastahili kupata mahitaji yake dukani. Napendekeza kila mtu awe na kadi ya ki electonic au line ya simu ambayo itakuwa inaingizwa taarifa za kwamba amefanya kazi na kutimiza wajibu kwa ufanisi na ataenda nayo dukani ambapo wataipitia kama ifanyavyo kazi atm au utumaji wa pesa kupitia simu

UKO WAPI USAWA?

Maisha ya mtu anayeishi ikulu na raia wa kawaida yatakuwa sawa. Wote wanakula wali, wote wanakula ugali na wote wanavaa vizuri. Raisi ana Gari na raia wa kawaida anasafiri bure. Hakuna kulipa bili za umeme, simu, maji, nyumba na leseni. Katika mfumo huu serekali huwa baba na raia ni watoto. Kama tunazalisha bure na bidhaa tunapewa bure. Kila kitu ni bure.